## Ushirikiano wa Ndani

## Mratibu wa Jimbo kuhusu Elimu kwa Wasio na Makao

Hati hii ilitayarishwa na Ofisi ya Msimamizi wa Mafunzo ya Umma, kwa kutumia lugha na nyenzo kutoka katika Kituo cha Taifa cha Elimu kwa Wasio na Makao. Hati hii imelindwa chini ya Creative Commons CC-BY. Kwa maelezo zaidi, tembelea k12.wa.us

Washington Office of Superintendent of
PUBLIC INSTRUCTION

Swahili

# *Unachohitaji Kujua ili Kumsaidia Mtoto Wako Shuleni*

## *Mwongozo kwa Wazazi, Walezi na Watunzaji*



Ikiwa familia yako iko katika hali ya kuishi ya muda mfupi au isiyoridhisha kutokana na kupoteza makao, huenda mtoto wako akastahiki haki na huduma fulani za elimu.

## Ustahiki wa Huduma za McKinney-Vento

Ikiwa familia yako inaishi:

- katika hifadhi;
- katika moteli au uwanja wa kambi kutokana na kukosa makao mbadala yanayoridhisha;
- katika gari, bustani, mahame, au kituo cha mabasi au garimoshi;
- kuungana na watu wengine kutokana na kupoteza makao au ugumu wa maisha;

mtoto wako anaweza kupata usaidizi kupitia sheria ya serikali kuu inayoitwa Sheria ya McKinney-Vento.

## Haki na Misaada ya McKinney-Vento

Watoto wako wanaostahiki McKinney-Vento wana haki ya

- kupata elimu ya umma ya bila malipo inayofaa.
- kujisajili shuleni mara moja, hata ikiwa hana hati zinazohitajika kawaida kwa ajili ya usajili.
- kujisajili shuleni na kuenda kwenye madarasa huku shule ikikusanya hati zinazohitajika.
- kujisajili katika shule ya karibu; au kuendelea kusoma katika shule ya awali (shule aliyosomea alipokuwa na makao ya kudumu au shule ambayo alijisajili mara ya mwisho), ikiwa hilo ni pendeleo lako.

  **Ikiwa wilaya ya shule inaamini kwamba shule unayochagua si kwa maslahi ya watoto wako, basi lazima wilaya ikupe maelezo ya maandishi ya msimamo wake na kukufahamisha kuhusu haki yako ya kukata rufaa ya uamuzi wake.*
- kupokea usafiri wa kuenda na kutoka kwenye shule ya awali, ukiomba huduma hii.
- kupata huduma za elimu zinazolingana na zile zinazopewa wanafunzi wengine, kulingana na mahitaji ya watoto wako.

- Sikiliza kile ambacho mtoto wako anakuambia na uzungumze kuhusu tatizo lolote alilo nalo. Pia unaweza kuzungumza kuhusu matatizo haya na mwalimu au mshauri wa shule.
- Mhimize mtoto wako ashiriki katika mambo kama vile michezo na muziki.

## Nyenzo kutoka NCHE

### Simu ya Usaidizi ya Bila Malipo: 800-308-2145 au homeless@serve.org

NCHE inaweza kueleza haki za shule za mtoto wako na kukuambia jinsi ya kuwasiliana na afisa wa ushirikiano wa ndani katika wilaya ya shule yako. Afisa wa ushirikiano wa ndani anaweza kusaidia kumsajili mtoto wako katika shule na kuhakikisha kwamba mtoto wako anapata usaidizi anaohitaji.

### Tovuti: http://nche.ed.gov

- Tovuti ya NCHE ina taarifa nyingi sana, ikiwa ni pamoja na ukurasa wavuti wa wazazi wanaotaka kumsaidia mtoto wao shuleni: https://nche.ed.gov/ibt/parent_res.php.

### Folda za Parent Pack Pocket

- Folda za Parent Pack Pocket ni folda ambapo unaweza kuweka rekodi na karatasi muhimu zinazohusiana na kusoma kwa mtoto wako. Folda pia inaeleza haki za elimu za mtoto katika hali za ukosefu wa makao.
- Agiza folda hizi bila malipo kwa kupiga simu 800-308-2145 au kutembelea: https://nche.ed.gov/online_order.php

- Je, kuna michezo, muziki, au shughuli nyingine zinazopatikana kwa ajili ya mtoto wangu?
- Je, ni vipi mtoto wangu anavyoweza kuenda kwenye ziara za nyanjani za darasa au kushiriki katika shughuli nyingine za shule ikiwa siwezi kumlipia?
- Je, kuna programu ya chekechea kwa watoto wangu wachanga?

## Je, ninaweza kufanya nini ili kumsaidia mtoto wangu shuleni?



- Hakikisha kuwa mtoto wako anaenda shuleni kila siku na anafika akiwa mepumzika na kula.
- Hakikisha kuwa kuna mazingira matulivu ili
- mtoto wako afanye zoezi la nyumbani; tenga muda wa kumsaidia mtoto wako kwa zoezi la nyumbani.
- Tazama mahitaji ya afya ya mtoto wako na shughulikia tatizo lolote mapema.
- Mwulize mtoto wako kile anachosoma shuleni. Mwambie akuelezee. Ukionyesha mvuto wa elimu ya mtoto wako, atajua kwamba ni muhimu.
- Msomee mtoto wako kila siku. Kwa watoto waliokomaa, tenga muda kila siku kwa ajili yako na mtoto wako ili kusoma pamoja kwa kimya. Zungumza kuhusu kile mlichokisoma.
- Mpongeze mtoto wako kwa kile anachokifanya vyema, kama vile kupata alama nzuri au kucheza kwenye timu ya michezo ya shule.

### Maswali Mazuri Huchochea Wasomaji Wazuri

Kuwauliza watoto kuhusu kile walichokisoma kutawasaidia kuwa wafikiriaji bora.

**Kwa hadithi (kubuni):**

- Je, ni nini kilichotendeka? Je, unadhani ni nini kitakachotendeka baadaye? Kwa nini?
- Je, mhusika mkuu ni nani? Je, unampenda? Kwa nini?
- Je, ungefanya kile alichokifanya? Ikiwa sivyo, ungefanya nini? Je, hadithi hii imekufanya uhisi vipi?

**Kwa makala ya taarifa (yasiyo ya kubuni):**

- Je, makala au sura ilihusu nini? Omba maelezo mengi iwezekanavyo.
- Je, unadhani lengo kuu la mwandishi lilikuwa gani?
- Je, ni sehemu ipi inayokuvutia zaidi?
- Je, kwa nini unadhani taarifa hii ni muhimu?

# Maswali Yanayoulizwa Sana

## Ninapohama, je, ninapaswa kumwacha mtoto wako katika shule ileile au nimhamishie kwenye shule ya karibu?

Kuhama kutoka shule moja hadi nyingine kunaweza kuwakera watoto. Wanalazimika kuwaacha rafiki na walimu wanaowajua na kuwazoea rafiki, walimu na madarasa mapya. Kwa sababu ya jambo hili, kwa kawaida huwa bora kwa mtoto wako kusalia katika shule ile ile (shule ya awali), hata ikiwa utahamia eneo tofauti.

Haya hapa baadhi ya maswali ya kufikiria wakati wa kuamua ikiwa mtoto wako anapaswa kusalia katika shule ileile au kuhamia shule mpya pale unapoishi:



- Je, mtoto wako ana umri gani?
- Je, makao yako unayoishi kwa sasa ni ya kudumu kwa njia gani? Je, unapanga kurejea karibu na shule ya awali au unadhani utakaa karibu na makao yako ya kuishi ya sasa?
- Je, mtoto wako anapenda shule yake ya awali? Mtoto aliyekomaa anayehisi kuipenda sana shule yake ya awali na/au anakaribia kuhitimu huenda akawa na changamoto kuzibadilisha shule.
- Je, mtoto wako ana wasiwasi kiasi gani kwa sababu ulihitajika kuhama? Je, kubadilisha shule kunaweza kuchosha zaidi?
- Je, kubadilisha shule kutasababisha mtoto wako kubaki nyuma katika shule na kupata alama mbaya?
- Je, huu ni wakati bora wa mwaka kwa mtoto wako kubadilisha shule, kama vile mwisho wa muhula au mwaka wa shule, baada ya mtihani, au baada ya tukio ambalo ni muhimu kwa mtoto wako?
- Je, mtoto wako atahitajika kutumia muda gani kuenda na kutoka katika shule ya awali? Safari ndefu inaweza kuwa na athari hasi kwenye kazi ya shule ya mtoto wako.
- Je, kuna masuala ya usalama ya kufikiria wakati wa kuchagua shule ambayo mtoto wako atasomea?

## Je, ikiwa mimi na shule hatutakubaliana kuhusu mahali ambapo mtoto wangu anapaswa kuenda shuleni?


Ikiwa wewe na shule hamtakubaliana, wilaya ya shule lazima ikuambie kwa njia ya maandishi sababu ya kudhani mtoto wako anapaswa kuenda kwenye shule tofauti na ile unayotaka. Wilaya pia itakuambia kwa njia ya maandishi jinsi unavyoweza kukata rufaa ya uamuzi huu. Mtoto wako anaweza bado kujisajili, kuhudhuria na kushiriki kikamilifu katika shule unayodhani ni bora kwake huku tofauti ikishughulikiwa.

## Je, ninaweza kuwasiliana na nani ili kusaidia kwa elimu ya mtoto wangu?



- Kila wilaya ya shule ina **afisa wa elimu wa ndani kwa wasio na makao.** Mtu huyu anaweza kukusaidia kuamua shule ambayo ni bora kwa mtoto wako na kuwasiliana na shule. Afisa wa ndani pia anaweza kumsaidia mtoto wako kupata vifaa vya shule, huduma za ziada na milo ya shule ya bila malipo; kupanga usafiri wa kuenda na kutoka kwenye shule ya awali; na kukusaidia kupata misaada ya jamii.
- Unapomsajili mtoto wako katika shule mpya, unapaswa kuomba kukutana na **m(wa)limu wake**. Pia unapaswa kuzungumza na mwalimu wa mtoto wako kila mara kuhusu jinsi anavyoendelea. Mfahamu angalau mwalimu mmoja kwenye shule ya mtoto wako vizuri sana ili uulize maswali kuhusu kazi ya shuleni ya mtoto wako na kumpa taarifa zitakazomsaidia mtoto wako kusoma.
- Mshauri **wa shule** anaweza kumsaidia mtoto wako kwa mabadiliko na changamoto. Shiriki na mtu huyu taarifa yoyote kuhusu jinsi mtoto wako anavyoendelea nyumbani, au mambo anayokabiliana nayo ambayo yanaweza kuathiri kazi ya shuleni.
- Watu wengine wazuri wa kujua ni **mwalimu mkuu wa shules, afisa wa mahudhurio, dereva wa basi, mhudumu wa jamii wa shule,**
- na **muuguzi wa shule.**
- **Wafanyakazi wote wa shule na wilaya ya shule** wanaweza kusaidia kuhakikisha kwamba mtoto wako anapata huduma zote anazohitaji ili kufanya vyema shuleni. Wewe ni mshirika muhimu katika elimu ya mtoto wako na unapaswa kushirikiana kama timu na shule na wilaya ya shule.

## Je, ni maswali gani ninapaswa kuuliza kuhusu huduma kulingana na Sheria ya McKinney-Vento??



- Je, afisa wa ndani wa elimu kwa wasio na makao ni nani? Je, ninaweza kuwasiliana naye vipi?
- Je, ni usafiri gani unaopatikana kwa mtoto wangu kusalia katika shule ileile (shule ya awali)?
- Ikiwa mtoto wangu atabadilisha shule, ni nani anayeweza kutusaidia kuhamisha rekodi hadi kwenye shule mpya haraka?
- Je, mtoto wangu anawezaje kupokea milo ya bila malipo shuleni?
- Je, mtoto wangu anawezaje kupokea vifaa vya shule bila malipo, ikihitajika?
- Je, ni nani anayeweza kusaidia ikiwa mtoto wangu anahitaji huduma za elimu maalum? Je, huduma hizi zinaweza kuharakishwa vipi?
- Je, ni usaidizi gani wa elimu unapatikana kwa mtoto wangu, kama vile programu za Title I au mafunzo ya baada ya shule?
- Je, ni programu gani zinaweza kusaidia kukuza talanta za mtoto wangu na kushughulikia mahitaji yake ya kipekee?

